**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA**

**KIZIDUO CHA MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA KAMATI YA FEDHA NA UTAWALA KILICHOFANYIKA TAREHE 29 NOVEMBA, 2021**

**(a) Wajumbe Waliohudhuria:**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mhe. Omary Kumbilamoto | - | Mstahiki Meya | - | **Mwenyekiti** |
| 2. Mhe. Saady Khimji | - | Naibu Meya | - | **Mjumbe** |
| 3. Mhe. Saada Mandwanga | - | Diwani wa Viti Maalum | | " |
| 4. Mhe.Tumike Malilo | - | Diwani wa Kata ya Bonyoka | | " |
| 5. Mhe. Kheri Kessy | - | Diwani wa Kata ya Kisutu | | " |
| 6. Mhe. Bonnah Kamoli | - | Mbunge Jimbo la Segerea | | " |
| 7. Mhe. Lucy Lugome | - | Diwani wa Kata ya Kisukuru- | | " |
| 8. Mhe. Stephen Mushi | - | Diwani wa Kata ya Kipunguni | | " |
| 9. Mhe. Moza Mwano | - | Diwani wa Viti Maalum | | " |
| 10. Mhe. Sultan Salim | - | Diwani wa Kata ya U/Mashariki | | " |
| 11. Mhe. Job Isaack | - | Diwani wa Kata ya Mzinga | | " |
| 12. Mhe. Azizi J. Mwalile | - | Diwani wa Kata ya Msongola | | " |
| 13. Mhe. Jerry W. Silaa | - | Mbunge Jimbo la Ukonga | | " |
| 14. Mhe. Mussa H. Zungu | - | Mbunge Jimbo la Ilala | | " |
| 15. BibiTabu F. Shaibu | - | Kaimu Mkurugenzi wa Jiji | | **Katibu** |

**(b) Wakuu wa Idara na Vitengo:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Bibi Benadeta Mwaikambo | - | Mkuu wa Idara ya Utawala na Utumishi |
| 2. Bw. Sije H. Lebi | - | Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika |
| 3. Bw. Majaliwa M. Andrea | - | Mkuu wa Idara ya Uvuvi na Mifugo |
| 4. Bibi Juliana E. Mhonyiwa | - | Mdhibiti Mkuu Ubora wa Shule (W) |
| 5. Bibi Subira A. Mwakibete | - | Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC |
| 6. Mwl. Sipora Tenga | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi |
| 7. Bw. Amen-Rabi Isaac | - | Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani |
| 8. Eng. John Magori | - | Mkuu wa Idara ya Ujenzi |
| 9. Bw. Ando Mwankuga | - | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |

10. Bw. RajabuNgoda - Mkuu wa Idara yaUhifadhi wa Mazingira na Udhibitiwa Taka Ngumu
11. Bw. Emmanuel Richard - Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipangomiji
12. Bibi Florah Luhala - Mkuu wa Kitengo cha Sheria na Usalama
13. Mwl. Mussa S. Ally - Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
14. Bw. Khalid J. Myaule - Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi
15. Bw. Kheri A. Sultani - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maji na Udhibiti Maji Taka
16. Dr. Nelson Mabruki - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya
17. Bw. Hashim Jumbe - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano
18. Bibi Jamila Kisaki - Kaimu Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
19. Bibi Fransisca F. Makoye - Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Vijana

**(c) Serikali Kuu:**

1. Bibi Charangwa S. Makwiro - Katibu Tawala Wilaya
2. Bw. George Anthony - Afisa Tarafa Ilala
3. Bw. Adrian G. Kishe - Afisa Tarafa Ukonga
4. Bibi Christina Kalekezi - Afisa Tarafa Kariakoo

**(e) Wakuu wa Sehemu:**

1. Bibi Rahma Shekwari - Afisa Utumishi
2. Bw. Kefa D. Gembe - Kaimu Afisa Biashara
3. Bw. Barnabas M. Kisai - Mratibu wa UKIMWI
4. Bibi Judith Nason - Afisa Sheria
5. Bw. Edwin Rwegoshora - Kaimu Afisa Mapato
6. Bibi Hamida Ahmed - Afisa Usafirishaji
7. Bibi Esther Kaboma - Kaimu Mratibu TASAF
8. Bibi Zuhura Mohamed - Mwangalizi wa Ofisi

**(f) Sekretarieti:**

1. Bibi Joyce. P. Decomarmond
2. Bibi Madaha Myalla

**MUHTASARI NA. 110/DCC.FEDHA/11/2021 – KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao saa 04:45 asubuhi.

**MUHTASARI NA. 111/DCC.FEDHA/11/2021 – KUSOMA NA KUPOKEA AGENDA.**

Katibu aliwasilisha jumla ya agenda 9 kama ifuatavyo:-

1. Kufungua kikao.
2. Kusoma na kupokea agenda.
3. A. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 28 Oktoba, 2021.
   B. Yatokanayo na kikao cha tarehe 28 Oktoba, 2021.
4. Taarifa ya Mapato na Matumizi ya Mwezi Oktoba, 2021
5. Kuhamisha fedha shilingi 5,100,000,000 kwenda kujenga vyumba vya madarasa 255 ya UVIKO – 19
6. Taarifa ya Maazimio ya Kikao cha Bodi ya Zabuni
7. Tarifa ya Ujenzi wa Mabucha – Machinjio ya Vingunguti.
8. Mengineyo kwa Idhini ya Mwenyekiti.
9. Kufunga kikao.

**Hoja:**

Hoja ilitolewa ya kuzipokea agenda na kuzijadili. Hoja iliungwa mkono na wajumbe.

**MUHTASARI NA. 114/DCC.FEDHA/11/2021 – KUHAMISHA FEDHA SHILINGI 5,100,000,000 KWENDA KUJENGA VYUMBA VYA MADARASA 255 YA UVIKO 19**

Mkuu wa Idara ya Idara ya Fedha na Biashara aliwasilisha taarifa ya akieleza kuwa Halmashauri ilipokea fedha za mpango wa maendeleo na mapambano dhidi ya UVIKO -19 ya madarasa 255 yenye thamani ya shilingi bilioni tano na milioni mia moja (5,100,000,000/=) Madarasa haya ni msambao na yanajengwa kwa kutumia mfumo wa "Force Account" . Madarasa yamegawanyika kijimbo kama ifuatavyo:- Jimbo la Ilala 70 Segerea 81 na Ukonga 104 na Kata zitakazo husika ni ishirini na mbili (22) na shule arobaini na moja (40), kutokana na mapokezi hayo kamati hii inaombwa idhini ya kuhamisha fedha hizo kwenda kujenga vyumba vya madarasa 255 ya UVIKO 19.

**Hoja:**

Hoja ilitolewa ya kuipokea taarifa na kuijadili. Hoja iliungwa mkono na wajumbe.

- **Hoja ya ziara ya kutembelea ujenzi wa madarasa ya UVIKO-19**

Mhe. Lucy Lugome alieleza kuwa, ni vema Kamati ya Fedha na Utawala ifanye ziara ya kutembelea utekelezaji ujenzi wa madarasa ya UVIKO-19

**Maelezo ya ufafanuzi:**

Katibu alieleza kuwa Managementi itaona utaratibu wa Ziara.

Mhe. Tumike Malilo alieleza kuwa, Kamati ya Fedha ni lazima itembelee ujenzi wa madarasa kabla ya kuhitimisha ujenzi tarehe 13/12/2021.

Mwenyekiti alieleza kuwa, Kamati ya Fedha iandaliwa Ziara ya kukagua mradi wa ujenzi wa Madarasaya UVIKO-19 tarehe 10/12/2021.

Baada ya majadiliano ya kina, Mhe Sultan Salim alitoa hoja ya kupitisha maombi ya kuhamisha fedha shilingi 5,100,000,000 kwenda kujenga vyumba vya madarasa 255 ya UVIKO – 19, hoja iliungwa mkono na Wajumbe.

**Azimio:**

Kamati ya Fedha na Utawala iliridhia kuhamisha fedha shilingi 5,100,000,000 kwenda kujenga vyumba vya madarasa 255 ya UVIKO – 19 pamoja na kuruhusu hatua zingine ziendelee.

**MUHTASARI NA. 118/DCC.FEDHA/11/2021 – KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga kikao saa 06:30 mchana.

***Umethibitishwa***

............................ ............................

***Katibu*** ***Mwenyekiti***

***Tarehe........................................***